# STANDARD SIX END TERM 3 EXAM, 2017
# KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo kisha ujaze nafasi zilizoachwa 1-15***

UKIMWI ni ugonjwa hatari sana. Tangu mwanzo mwanzo wa miaka __1__ themanini,ugonjwa huu umeleta shida __2__ sana duniani. Ugonjwa wa UKIMWI huusabibishia mwili wa mgonjwa kuwa __3__. Watu wengi __4__ kutokana na ugonjwa huu. Watoto wengine nao huwapoteza wazazi wao na kubaki __5__. Ni lazima __6__ ili __7__ ugonjwa huu hatari.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | wa | za | la | ya |
| 2. | mkubwa | likubwa | kubwa | makubwa |
| 3. | mdhaifu | dhaifu | wadhaifu | kidhaifu |
| 4. | wameiaga dunia | wameaga dunia | wanaaga dunia | wanaiaga dunia |
| 5. | yatima | mjane | wajane | mayatima |
| 6. | tuwe macho | tuwe wengi | tuangaliwe | tuone |
| 7. | tusipewe | tusilete | tusiambukizwe | tusiletewe |

Teknolojia ni hali ya kutumia vyombo vya kisasa kuharakisha kazi.Teknolojia imezidi __8__ na kuwa yenye __9__.Vyombo mbalimbali vimeundwa ili kuharakisha mawasiliano kote duniani. Vyombo hivi ni kama vile __10__ kompyuta,televisheni,rununu na __11__.Kompyuta, __12__, imesaidia kuleta mabadiliko __13__ katika kampuni zetu na kufanya kazi kuwa __14__.Rununu huwaleta watu pamoja kwa kuwasiliana __15__.Twaomba serikali yetu iendelee kuboresha na kupanua teknolojia.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. | kuimarisha | kuimarika | kuimarishwa | kuamrishwa |
| 9. | faida mingi | manufaa nyingi | manufaa mengi | faida mengi |
| 10. | , | ! | . | : |
| 11. | nyingine nyingi | vingine vingi | mengine mengi | zingine nyingi |
| 12. | kwa mfano | na | piya | nasi |
| 13. | nzuri | njema | zuri | mema |
| 14. | nyepesi | raisi | wepesi | rais |
| 15. | kila siku | mara | mara kwa mara | kila saa |

***Katoka swali la 16-30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo.***

16. Ni sentensi gani iliyo na kiambishi **KI** cha udogo?
   A. Tumekisoma kitabu cha hadithi
   B. Tukiandika insha nzuri mwalimu atatupongeza
   C. Kiatu hicho ndicho cha mtoto
   D. Kigombe changu kimeumia kiguu

17. Kanusha sentensi ifuatayo;
   Wewe umenisaidia sana.
   A. Wewe hujanisaidia sana
   B. Wewe haujanisaidia sana
   C. Wewe hutanisaidia sana
   D. Wewe hautanisaidia sana

18. Nyambua kitenzi **fagia** katika kauli ya kutendea
   A. fagiwa B. fagiliwa
   C. fagiia D. fagilia

19. Chagua jina la ukoo lililoambatanishwa vyema na maana.
   A. Mpwa – mtoto wa dada
   B. Mjomba – kaka wa baba
   C. Amati – dada wa mama
   D. Mbiomba – kaka wa mama

20. Kamilisha tashbihi;
   Waswallah ni mwaminifu kama
   A.mbwa B.mchana
   C.usiku D.paka

21. Ni sentensi gani iliyo na kivumishi halisi?
   A. Mtoto huyu ni mwerevu
   B. Wakati wowote naweza kukusaidia
   C. Watoto wawili wameonekana
   D. Rozi ndiye mwanafunzi wa nne

22. Ni nini wingi wa:
   Nimeula mkate wangu
   A. Tumekula mikate yetu
   B. Nimeila mikate yangu
   C. Nimezila mikate zangu
   D. Tumeila mikate yetu

23. Kamilisha methali
   Chanda chema
   A. marejeo ni ngamani
   B. usimwangalie usoni
   C. huvishwa pete
   D. humrukia

24. Mkulima ni kwa lima kama vile mlinzi ni kwa
   A. linzi B. lia
   C. kulinda D. linda

25. Tumia amba:
   Kijana aandikaye ndiye Mugo
   A. Kajana atakaye andika ndiye Mugo
   B. Kijana ambaye anaandika ndiye Mugo
   C. Kijana ambaye anayeandika ndiye Mugo
   D. Kijana ambaye aandikaye ndiye Mugo

26. Chagua kiwakilishi katika sentensi hii
   Niitie Asmini nimtume,huyu amekataa kuenda
   A. huyu B. huyu
   C. Asmini D. kuenda

27. Ni chombo gani kisichopatikana sebuleni?
   A. Dari B. Kochi
   C. Zulia D. Manati

28. Ni nomino gani iliyoorodheshwa katika ngeli sahihi?
   A. pua - LI-YA
   B. kiziwi - A-WA
   C. jezi - LI- YA
   D. mtume - U-I

29. Mwalimu alipigwa kalamu kwa uzembe wake. Ndiko kusema?
   A. Alipewa zawadi
   B. Alipeana kalamu
   C. Alifutwa kazi
   D. Aliandikiwa barua

30. Hospitalini, watu husubiri zamu zao katika:
   A. Pambajio B. Mochari
   C. Wodi D. Thieta

***Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.***

Hamjambo wanafunzi? Hamjambo tena? Jina langu ni Ustadh Utubora kutoka katika shule ya msingi ya Elimika. Leo hii nina furaha kubwa kujumuika nanyi hapa penu shuleni. Ni wangapi wana furaha adhuhuri ya leo? Asanteni sana.

Nimeandamana na Bi Subira ambaye ni afisa katika shirika linalotetea haki za watoto. Nawaomba muwe wasikivu na wenye subira.

"Hamjambo watoto wazuri? Kama mlivyoambiwa mimi ni Bi Subira kutoka shirika la haki za watoto. Nataka kuzungumza juu ya maisha yenu. Siku hizi kuna visa vingi sana vya watoto wadogo kama nyinyi kudhulumiwa. Leo nitawaeleza jinsi ya kujiepusha na dhuluma hizo.

Kwanza msikubali kuitwa na watu msiowajua na mkawafuata. Huenda wakawa wabaya. Vile vile, msikubali chakula cha aina yoyote kutoka kwa watu msiojua. Chakula na kinywaji chako wafaa ukipate kutoka nyumbani kwenu.

Jingine muhimu ni kwamba, kila mara uwe na wenzako unaowajua unapokuja shuleni au kuenda kokote. Unapotaka kuenda mahali, hakikisha kuwa umemwomba mzazi wako ruhusa. Je, kati yenu nyote, ni nani hupenda kuingiaingia katika nyumba za watu? Kwa kuwa ni wachache wenu, ningependa kuwashauri kuwa msikubali kuingia katika nyumba za watu msiojua.

Ni muhimu kutosheka na hali yako ya maisha na ya maisha ya wazazi wako. Iwapo hamna uwezo mkubwa, msijali. Hiyo ni bora kuliko kuombaomba kutoka kwa watu. Msiwe watu wa kudanganywa kwa urahisi.

Namalizia hotuba yangu kwa kuwashauri kwamba ni vyema kuwatii wazazi na walimu wenu. Licha ya haya, ni vyema kumheshimu kila mmoja na pia kujiheshimu. Asanteni."

31. Wanafunzi waliongeleshwa saa ngapi?
    - A. Saa sita mchana
    - B. Saa mbili asubuhi
    - C. Saa moja jioni
    - D. Saa tatu usiku

32. Ni sentensi gani iliyo ya kweli kulingana na ufahamu?
    - A. Bi Subira alikuwa mwalimu katika shule ya Elimika.
    - B. Watoto walizungumziwa na walimu wao
    - C. Bi Subira hakuwa mwalimu
    - D. Ustadh Utubora na Bi Subira walikuwa walimu

33. Kabla ya Bi Subira kuanza maongezi yake, Ustadh Utubora aliwataka wanafunzi:
    - A. walete viti
    - B. wampigie makofi
    - C. watoe maoni
    - D. wasikilize kwa makini

34. Kwa nini watoto walishauriwa wasiwafuate watu wasiowajua?
    - A. Huenda wakapewa peremende
    - B. Watu hao wanaweza kuwapoteza
    - C. Wanaweza kupotea wakiwafuata
    - D. Baadhi ya watu si wazuri

35. Msemaji anawashauri watoto wapate chakula kutoka wapi?
    - A. Kwao shuleni
    - B. Kwao nyumbani
    - C. Kwa majirani zao
    - D. Kwa rafiki zao

36. Kulingana na taarifa, wanafunzi waliokuwa na tabia ya kuingia katika nyumba za watu wasiowajua;
    - A. Hawakuwa wengi
    - B. Waliadhibiwa vikali
    - C. Walikuwa wengi sana
    - D. Walikuwa zaidi ya nusu ya idadi nzima

37. Watoto walishauriwa juu ta mambo mangapi?
    - A. Sita
    - B. Matano
    - C. Manne
    - D. Saba

38. Watoto walipoambiwa;
    " Ni muhimu kutosheka na hali yako" msemaji alimaanisha nini?
    - A. Wasipende kupewa zawadi na mtu yeyote
    - B. Wafurahie walivyo hata vikiwa duni au vibaya
    - C. Siku zote wasipendezwe na maisha mema
    - D. Wawe wakiombaomba kwa rafiki zao

39. Mazungumzo ya aina hii ni;
    - A. matangazo
    - B. hotuba
    - C. hadithi
    - D. maelezo

40. Ni methali gani inayofaa paragrafu ya mwisho?
    - A. Leo ni leo, msema kesho ni mwongo
    - B. Haraka haraka haina baraka
    - C. Siku za mwizi ni harubaini
    - D. Heshima si utumwa



Compiled by **Schools Net Kenya | P.O. Box 85726 – 00200, Nairobi |**
**Mob. 0711 88 22 27 | Email: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com**

***Soma kisa kifuatacho kisha ujibu 41-50.***

Shule ya msingi ya Makali ilikuwa na takribani wanafunzi mia sita tisini na sita. Miongoni mwao alikuwa kijana mmoja aliyeitwa Alvin. Alvin alikuwa katika darasa la tano mashariki. Kijana huyo alikuwa mtanashati tena sana. Licha ya kuumbwa akaumbika, kijana mwenyewe goigoi kupindukia. Ugoigoi wake ulimfanya akose kuoga, kujifulia na wakati mwingini hata kupiga mswaki kulimshinda.

Siku moja baada ya kula chajio, aliamua kuenda kulala mapema. Hakulala sana. Ghafla bin vuu, aliamshwa na maumivu makali ya tumbo. Alimwita mama yake huku akilia kwa uchungu mno. Mama mtu kusikia hivyo, aliamka haraka kama umeme na kumpeleka katika hosipitali ndogo iliyokuwa karibu na hapo pao.

Kabla ya kufika huko, Alvin alikuwa ametapika na kuendesha sana. Walipofika, tabibu alimhudumia haraka ili kuyaokoa maisha yake. Alipochunguzwa damu, choo, matapishi na mkojo, tabibu alisema wazi kuwa aliugua ugonjwa wa kipindupindu. Alilazwa humo hosipitalini kwa majuma mawili hadi alipopata nafuu na kuruhusiwa kurudi nyumbani. Alipokuwa akiondoka hosipitalini, tabibu alimweleza kijana Alvin umuhimu wa kuwa safi. Alinweleza kuwa tukiwa safi ama tukiishi katika mazingira safi hatutapatwa na magonjwa mengi kama vile homa ya matumbo. kuendesha. kipindupindu na kadhalika.

Kuanzia siku hiyo, Alvin alikomesha tabia yake ya uvivu na kufuata maagizo ya tabibu wake. Baadaye akawa mwanafunzi mwema na mwenye afya njema.

41. Shule iliyotajwa ilikuwa na karibu wanafunzi;
    A. 696 B. 966
    C. 669 D. 996

42. Katika paragrafu ya kwanza,tunadokezwa kuwa Alvin alikuwa na tabia gani?
    A. Ya uvuvi
    B. Ya bidii
    C. Ya kukataa kuoga
    D. Ya uvivu

43. Chajio ni chakula cha wakati gani?
    A. Asubuhi
    B. Mchana
    C. Jioni
    D. Adhuhuri

44. Ni nini kilichomfanya Alvin kuamka alipokuwa amelala?
    A. maumivu makali ya mwili
    B. alikuwa akiwangwa na kichwa
    C. alikuwa akisokotwa na tumbo
    D. tumbo lake lilimwasha sana.

45. "…….haraka kama umeme….." ni :
    A. Nahau
    B. tashbihi
    C. kitendawili
    D. methali

46. Mama wa Alvin alimpeleka mwanawe katika hosipitali ndogo, yaani:
    A. zahanati
    B. wodi
    C. mochari
    D. maabara

47. Ni nani aliyempa Alvin mawaidha ya usafi?
    A. mama yake
    B. rafiki yake
    C. mganga wake
    D. mwalimu wake

48. Kati ya vilivyotajwa, ni gani hakikuchunguzwa?
    A. mkojo
    B. kinyesi
    C. matapishi
    D. jasho

49. Ni ugonjwa gani haujatajwa katika taarifa?
    A. kipindupindu
    B. malale
    C. kuendesha
    D. homa ya matumbo

50. Alvin alilazwa kwa muda wa siku ngapi?
    A. kumi
    B. kumi na nne
    C. sababu
    D. sitini